Pakua nakala hii ya PDF kwenye www.jw.org/sw

Yosefu Katika Nchi ya Misri

MWANZO SURA YA 39-40

Chagua mazoezi yanayofaa mahitaji na mapendezi ya mtoto wako. Fanyeni mazoezi hayo mkiwa familia.

SOMA MWANZO SURA YA 39-40

Kisha, someni hadithi ya Biblia iliyochorwa (kwenye Intaneti au kwenye karatasi iliyochapishwa), na mzungumzie maswali yaliyo mwishoni mwa hadithi.

JARIBU KUFANYA HIVI: Waombe watoto wako wajifanye kuwa waandishi wa habari wanaoripoti tukio hilo. Kisha wajifanye kuwa wanawahoji wahusika wakuu na mashahidi walioona jambo hilo.

Katika lugha fulani, mnaweza kusikiliza drama ya Biblia ya hadithi hii yenye kichwa *"Preserving Life in Time of Famine"* (Kuhifadhi Uhai Wakati wa Njaa). Drama hiyo iliyorekodiwa inatia ndani matukio yatakayozungumziwa katika hadithi zilizochorwa za wakati ujao. Unaweza kupakua drama hiyo kutoka kwenye Tovuti ya www.jw.org. Tafuta chini ya PUBLICATIONS > DRAMAS.

MAZOEZI ZAIDI UNAYOWEZA KUCHAPISHA



MAZOEZI YA PICHA

KUNA TOFAUTI GANI? Someni tena Mwanzo 40:16, 17. Kisha, waombe watoto wadogo (miaka 3 hadi 5) watafute mambo matatu yaliyo tofauti kati ya picha hizo mbili, waandike majibu yao kwenye mistari, na wapake rangi picha sahihi.

MAZOEZI YA KUJIFUNZA

NI MAMBO GANI YANAYOFANANA? Waombe watoto wakubwa (miaka 6 hadi 10) wasome madokezo na kuandika kwenye mistari mambo yanayofanana kati ya Yosefu na wahusika wengine wa Biblia.

KUSANYA NA UJIFUNZE

KADI YA MHUSIKA KATIKA BIBLIA: Soma mambo machache kumhusu. Uliza maswali yaliyo kwenye kadi. Kwa kutumia kadi hiyo na kadi nyingine mlizo nazo, msaidie mtoto wako ataje wahusika wa Biblia wanaopatikana katika kitabu cha Mwanzo. (Dokezo: Kitabu cha Mwanzo kinahusisha matukio ya mpaka mwaka wa 1657 K.W.K.)

www.jw.org © 2013 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania